



Kuhakikisha haki katika data/takwimu **#DataValues Manifesto**

Utomizi wa data kutatua matatizo ya jamii daima imekuwa muhimu kwa maendeleo ya binadamu. Kuanzia uchapishaji hadi utengenezaji wa chanjo, data mpya, uchambuzi na maarifa yamewawezesha watu kuandika upya sheria na kuboresha maisha kwa kiasi kikubwa.

Lakini, ubinadamu unapokabiliana na changamoto zilizopo za mabadiliko ya hali ya hewa, uhaba wa chakula, na magonjwa ya milipuko, hatutumii data bora zaidi inayopatikana kushughulikia shida mbaya zaidi. Kupungua kwa uaminifu, kutengwa, ukosefu wa usawa, na njia zilizopitwa na wakati za kufanya kazi kunaleta vizuizi kati ya data na wale wanaonufaika zaidi nayo.


Data inahitaji kuhudumia kila mtu, na kuipata kwa usahihi ni jitihada za kisiasa na kijamii kama vile ni za kiufundi. Ni lazima tujenge mifumo ya data inayosaidia na kuwawezesha watu, badala ya kuwadhuru na kuwatenga. Hili linahitaji mabadiliko katika njia tunazounda, kukusanya, kufadhili, kudhibiti na kutumia data.

Harakati ya #DataValues inataka hatua za haraka zichukuliwe ili kuunda siku zijazo za haki za data. Mashirika, serikali na watu lazima wachukue hatua sasa na kwa pamoja ili kuleta mabadiliko haya.

Itachukua nini?

1.


Saidia watu kuweza kuchangia jinsi wanavyowakilishwa katika data.



Watu lazima wawe na sauti katika muundo na ukusanyaji wa data unaoathiri maisha yao. Kila mtu anastahili mahitaji yake, vipaumbele, na uzoefu—kama anavyofafanua—kunaswa katika data.

2.


Wekeza ushiriki wa umma kuendeleza uwajibikaji.



Watu lazima wajumuishwe katika maamuzi yanayohusiana na utumiaji wa data. Hii ni muhimu kuwajibisha viongozi, kuwalinda watu dhidi ya madhara, na kuboresha maisha.

3.

Weka usawa zaidi kwa ujuzi wa data.



Kila mtu, kila mahali lazima apate ujasiri wa kujihusisha na kutumia data. Uaminifu wa data ulioenea ni msingi wa mustakabali mzuri wa data.

4.

Unda tamaduni za uwazi, kushiriki data na matumizi.



Viongozi wote lazima wawekeze katika kuimarisha tamaduni za matumizi ya data. Uzoefu chanya unaorudiwa wa kudhibiti, kushiriki na kutumia data kwa manufaa ya umma utajenga uaminifu.

5.

Kufadhili mifumo ya data iliyo wazi na inayoleta mabadiliko ili watu wote washiriki kupata manufaa ya data.



Serikali na wafadhili lazima watoe ufadhili zaidi kwa mifumo ya data inayounga mkono hatua na kukuza ushirika na ushirikishwaji kuanzia mwanzo hadi mwisho.